

1. Jina na Maelezo ya Mradi

- **Jina la Mradi:** Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience – EBARR in Tanzania).
- **Maelezo:** Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) inatekeleza mradi unaohusiana na mabadiliko ya Tabianchi. Mradi huu unaitwa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini. Mradi huu ni wa miaka mitano (2018 – 2022). Wilaya zinazotekeleza mradi ni:- Kishapu (Shinyanga), Mvomero (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma), Simanjiro (Manyara) kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Visiwani mradi unatekelezwa katika Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja.
- **Mfadhili wa Mradi:** Mradi huu umefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Nchi Maskini Duniani (Least Developed Countries Fund - LDCF) kupitia Mfuko wa Mazingira Duniani (Global Environment Facility – GEF). Masimamizi wa Mradi au *Implementing Agency* ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (United Nations Environment Programme – UNEP).

2. Lengo la Mradi: Kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini Tanzania kwa kuimarisha mifumo ikolojia.

Kupitia mradi huu wananchi watajengewa uwezo wa kuhimili changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha uwezo wao wa uvumilivu na uwezo wa mifumo ikolojia inayowazunguka kusaidia katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, wananchi katika maeneo ya mradi watajifunza njia mbalimbali mbadala (mfano: kilimo rafiki kwa mazingira CSA) za kujipatia mahitaji katika hali inayobadilika kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

3. Maeneo ya Mradi: Mradi unatekelezwa katika Wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A, (Kaskazini Unguja).

4. Kazi za Mradi:-

- i. Kubuni na kuendeleza muundo na mfumo wa usimamizi katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia nyenzo rahisi zinazopatikana (Adaptation Knowledge Management System - AKMS);
- ii. Kuandaa mafunzo kwa Wataalam (Training of Trainers - ToT) toka maeneo mbalimbali ambao watatumika kufundisha wataalam wengi zaidi kuhusu masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupitia mfumo ikolojia;
- iii. Kufanya tathmini ya hatari ya mabadiliko ya tabianchi (Vulnerability and Impact Assessment - VIA) kwenye maeneo ya mradi na kupendekeza namna bora ya kutekeleza kazi hiyo au kuiboresha;
- iv. Kutekeleza Kilimo rafiki kwa Mazingira kinachoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculture CSA) kama vile umwagiliaji unaozingatia hifadhi ya maji (Conservation based irrigation), uvunaji wa maji ya mvua, kilimo cha mzunguko, Skimu za Umwagiliaji n.k.;
- v. Kuboresha uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kuingiza kipato kwa wananchi/vikundi mbalimbali vya wahanga wa mabadiliko ya tabianchi hususan wanawake katika maeneo ya ufugaji mifugo, nyuki, samaki n.k. (income generating activities);
- vi. Kufanya utafiti kwenye maeneo ya mradi (Baseline study) na kujua hali halisi ili baada ya mradi kutekelezwa upimaji wake uzingatie mabadiliko halisi yaliyoletwa na mradi;
- vii. Mafunzo kuhusu namna ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia njia ya Mifumo Ikolojia (EbA approaches) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Jamii katika maeneo ya mradi;
- viii. Kuchimba malambo. Majosho na kuvuna maji ya mvua;
- ix. Kuanzisha shughuli za ushonaji wa nguo, utengenezaji manukato, mafuta n.k. kwa vikundi vya akina Mama;

- x. Kushirikiana na jamii za maeneo ya utekelezaji mradi, kutenga maeneo lindwa (no-take zones) ili kusaidia kurudi kwa uoto wa asili kwenye maeneo yaliyoharibika;
- xi. Kwa kushirikiana na jamii, kuandaa Mipango mipya ya matumizi ya ardhi na usimamizi inayohimili misimu na mabadiliko ya tabianchi;
- xii. Kukarabati au kuongoa (rehabilitation) nyanda za malisho (rangelands) zenye ukubwa wa hekta 6,000;
- xiii. Kuanzisha kilimo cha majani kwa ajili ya mifugo;
- xiv. Kuongoa lindimaji (catchments) kwa kutumia mimea ya asili katika eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000;
- xv. Kufanya ukarabati wa kingo za mito (riverbanks rehabilitation) katika eneo la hekta 200; na
- xvi. Kuanzisha na kuhamasisha utengenezaji na matumizi ya majiko banifu na sanifu, na teknolojia bora ya uzalishaji mkaa ili kupunguza matumizi makubwa ya misitu.